## GREDI YA SITA

## MASWALI

**Swali la 1 hadi la 5.**
Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

*(Babu ameketi chini ya mti akisoma gazeti. Analiweka gazeti kando anapomwona Muli)*
Muli: (akimsogelea Babu) Shikamoo Babu?
Babu: (kwa tabasamu) Marahaba mjukuu wangu! Habari za shule?
Muli: Njema babu! (kimya) Babu, nikwambie kitu?
Babu: Naam, niambie mjukuu wangu.
Muli: Wenzangu walinichagua kuwa kiranja wa darasa.
Babu: Hongera! Jambo zuri.
Muli: (akijikuna kichwa) Lakini Babu, sijui ninastahili kufanya nini ili niwe kiongozi bora.
Babu: Aha! Muli, sikiliza, ili kuwa kiongozi bora unastahili kuwa na maadili.
Muli: Ooh! Maadili…
Babu: Naam mjukuu wangu. Unaweza kuonyesha maadili kwa namna mbalimbali. Kwanza uwahudumie wenzako bila kuwabagua.
Muli: Kweli Babu, ninafikiria pia ninastahili kuwaonyesha upendo.
Babu: Ndiyo Muli. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwajali na kuwasaidia wenzako.
Muli: Kweli Babu! Ninaona kwamba heshima, umoja na ushirikiano pia ni mambo muhimu.
Babu: Haswa! Heshima si utumwa. Je, unaweza kuonyesha heshima kwa njia gani?
Muli: (Kwa ujasiri) Kwa kuwaamkua wote na kusikiliza wanayoyasema.
Babu: Vyema! Unastahili pia kuwa mwaminifu. Tunaonyesha uaminifu kwa kusema ukweli na kufanya mambo inavyostahili.
Muli: Asante babu! Hakika umenifunza mengi.

1. Muli alipoulizwa na babu kuhusu habari za shule, alimjibu
   A. Naam
   B. Njema
   C. Shikamoo
   D. Marahaba
2. Maneno yafuatayo yametumiwa katika mazungumzo. Lipi halionyeshi adabu?

A. Karibu
B. Naam
C. Asante
D. Kweli

3. Ni jibu lipi linaloonyesha maadili ambayo Babu alimfunza Muli?
    A. Kuhudumia, kuheshimu na kusikiliza.
    B. Kuamkua, kusikiliza na kujali.
    C. Kujali, kusaidia na kuwa mwaminifu.
    D. Kuwa na heshima, kushirikiana na kusaidia.
4. Unafikiri Muli atafanya nini baada ya kumuaga Babu?
    A. Atafurahia kuwa kiongozi shuleni.
    B. Atazingatia mawaidha ya babu.
    C. Atawaeleza wenzake kuhusu alivyokutana na babu.
    D. Atawapongeza wenzake kwa kumchagua kuwa kiranja
5. Neno maadili limetumika katika mazungumzo maana yake ni
    A. Mienendo mizuri inayofaa kuzingatiwa na mtu.
    B. Maonyo ambayo hutolewa mtu anapokosea.
    C. Matendo ambayo mtu huwafanyia wenzake.
    D. Mitindo mipya inayofuatwa na mtu.

**Soma kifungu kisha uiibu maswali.**

Ajira ya watoto ni kazi ambazo zinawatumia na kuwaathiri vibaya watoto kati ya miaka mitano hadi kumi na saba. Kwa namna fulani, watoto huathirika kiakili, kimwili,kimakazi na kimaadili, pia; ajira hizi ni kizuizi cha watoto hawa kupata elimu. Mateso yanayowapata watoto katika ulimwengu wa ajira ya watoto duniani ni mengi. Ajira hizi huweza kuwa za nyumbani kwa watu wengine, mashambani au viwandani. Kazi wanazozifanya watoto hawa ni pamoja na kulisha mifugo, kuchimba mawe, kufyatua matofali, kuchonga mawe, ujenzi wa barabara, kuvuta au kusukuma mikokoteni na za ndani ya nyumbani. Zote hizi ni kinyume na haki za binadamu kwa jumla.

6. Tumearifiwa kuwa ajira ya watoto huweza kuwaathirl watoto

A. kimaadili, kimakazi na kidini

B. kiakili, kimavazi na kimwili

C. kimakazi, kiakilii na kimaadili

D. kiakili, kimwili na kiukoo

7. Kulingana na kifungu, ajira ya watoto haiwezi kuwa

A. nyumbani kwa wengine

B. katika viwanda

C. mashambani

D. shuleni

8. Haki za binadamu hazimkubali mtoto

A. kuosha vyombo nyumbani kwao

C. kulifagia darasa lao

B. kuvuta mikokoteni kwa malipo

D. kufua sare zake.

**<u>Soma kifungu kisha ujibu maswali.</u>**

Ilibidi chifu wa kijiji chetu aïtane mkutano wa hadhara. Wananchi wa kijiji cha

Marumo waliapa kuwasaka na kuwaangamíza wezi wote kijijini. Usiku huo ukweli wa methali siku za mwizi ni ______________ ulionekana wazi. Walimkuta Bwana Fitina akivuna mahindi ya jirani yake. Walimchapa vibaya na kumpeleka polisi.

9. Je, ni shinda gani ilimfanya chifu aitanemkutano wa hadhara?

A. Ili kuwadhibu wezi

B.Ili kuwasaka wezi

C. Ili kuwaua wezi

D. Ili kuwachoma wezi

10. Je makala haya yanaongea juu ya kijji gani?

A. Cha Chifu

B. Cha mavuno

C: Cha wezi

D. Cha Bidi

11. Ni kina nani waliapa na kuangamiza wezi?

A. Wanakijiji

B. Majirani

C.Wezi

D. Chifu

12. Kamilisha methali. Siku za mwizi ni

A. chache B. kifo

C. arubaini D. hamsini

**<u>Soma kifungu kisha ujibumaswali</u>**

Kila Jumamosi, Mama yetu huenda sokoni na kutuachia shughuli za kutekeleza nyumbani. Mimi ndimi Mwanambee. Mama huniambia niwe mwangalizi akiwa na shughuli za nje. Kaka zangu wawili na dada zangu watatu hunisaidia kufanya shughuli za ndani. Ni watiifu. Daima hawakaidi maagizo yangu. Jumamosi moja, mama aliondoka kwenda sokoni kama alivyozoea. Tuliamua kuzigawa kazi ili tumalize kabla hajarejea. Niliwaambia dada zangu wafue, wasafishe nyumba na kutayarisha chamcha. Kaka zangu walipaswa kufyeka nyasi ndefu na kuulenga ua. Ghalla, nilimsikia mbuzi wetu akilia lo! Ni nani atakayewashughulikia wanyama hawa? Nikauliza.

13. Je, familia ya kina mwandishi ina jumla ya watu wangapi?

A. Saba B. Sita

C. Wanane D. Watano

14. Kulingana na ufahamu, ni kweli kusema kuwa watoto katika familia hii

A. hufanya shughuli zao kwa ushirikiano

B. kila mara hufanya shughuli zao kwa haraka

C. wamejawa na kiburi na majivuno

D. ni wazembe kupindukia

15. Mwishowe, ni nani ambaye aliwashughulikia wanyama wa kina mwandishi?

A. Mwandishi mwenyewe

B. Kaka wa mwandishi

C. Dada wa mwandishi

D. Hatujaelezwa

**<u>Jaza pengo</u>**

Baada ya ___16___masomo, mwama alitokomea nakuyoyomea_17_Mambo.

Binti_18_aliyelelewa_ 19 __ya utajiri si umaskini yaani_20_yamkini

aliamba, "Ni wengi wamesoma na vyeti wanavyo na lo! Hawana_21__wala bazi.

Sisomi tena. La saba lanitosha. La nane __ 22__sitalisoma! Mji mkuu naja!"

16. A. kumaliza B. kuyaasi C. kuyasoma D. Kuyaenda

17. A. jijini B. mjini C. Kariani D. Kitongojini

18. A. hawa B. huo C. huyu D. yule

19. A. maishani B. baitini C. aulani D. aushi

20. A. ulalahoi B. ulalahai C. ulalaheri D. uchochole

21. A. maisha B. chumo C. bahati D. kazi

22. A. sijui sitambui B. kutwa kucha C. liwe liwalo D. ashakum si matumi

**Jibu kulingana na maelezo**

**Kamilisha sentensi**

23. Jabibu alitupatia ________ mazuri.

A. Timba B. Matibaa
B. Matibabu D. Utibu

24. Kijana mwizi alifungwa kwa ajili ya ___________ wake.

A. wezi B. mwizi

C. uwizi D. wizi

25. Jina linguine la ukuta ni.

A. Kiambaza B. kuta

C. ukumbi D. msonge

26. **Tashbihi**

Popo amekonda kama ____________

A. sindano
B. ng'onda
C. kijiti
D. kasuku

27. Jiwe, lilianguka majini __________

A. tang'

B. pu

C. chumbwi

D. twa.

28. Kiulizi:

**Utakuja kwetu**________?

A. wapi B. gani

C. lini D. yupi